# Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Riwaya Teule za Zainabu Burhani

Rose Mavisi

**Ikisiri**

Makala hii inashughulikia usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya za Zainabu Burhani. Riwaya hizo ni *Mali ya Maskini* (1981), *Mwisho wa Kosa* (1987) na *Kipimo cha Mizani* (2004). Burhani katika kusawiri wanawake anapiga vita mfumo dume ijapokuwa haepuki athari zake kabisa. Burhani anasawiri vizazi tofauti vya wanawake; kizazi kichanga chenye shime ya kupambana ili kiweze kujikomboa, na kizazi kikongwe kinachokubali hali ilivyo. Nadharia iliyoongoza makala hii ni Unisai wa Kiafrika. Nadharia hii hueleza matatizo yanayowakabili wanawake wa Kiafrika na jinsi wanavyoweza kujiepusha nayo. Kwa mujibu wa nadharia hii Burhani amewasawiri wanawake kwa mtazamo hasi. Jamii nayo pia imewaweka wanawake katika nafasi ya pili baada ya wanaume. Haya yote yanasababishwa na itikadi ya mfumo dume, mazingira na malezi inayowafanya wanawake hawa kuikubali hali yao. Hata hivyo kuna matumaini kupitia kizazi kichanga cha wanawake ambao wanajitahidi kuikata minyororo hii.

## 1.0 Utangulizi

Waandishi mbalimbali wa Kiswahili wamemsawiri mwanamke kwa namna tofauti tofauti hasa kulingana na tajiriba zao katika maisha mbalimbali na mielekeo au kaida za jamii zao (taz. Chesaina, 1987; Ndungo, 1985; Kimani, 2003; Gitau, 2005). Kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili zimeandikwa na wanaume. Mtazamo wa wanawake pamoja na tajiriba zao za maisha zipo katika kazi hizi ingawa ni hasi. Usawiri huu wa wahusika wanawake unatokana na tajiriba ya kiume na mwanamume anavyotarajia mwanamke kuwa. Hii ni kwa sababu wanaume na wanawake aghalabu huathiriwa na maisha ya kijamii kwa njia tofauti kwani misingi na kaida za kijamii zimejengwa ili kukidhi na kuendeleza tofauti hizo.

Suala la mwanamke limekuwa la mjadala muhimu katika karne hii. Kuna baadhi ya waandishi katika fasihi ambao wameona umuhimu wa kuwasawiri wahusika wa kike wanaoweza kuigwa na umma hasa kutokana na uwezo wao. Katika uhalisi wa maisha tunayaona haya yakijitokeza katika jamii zetu. Wanawake halisi katika janibu hizi wanatekeleza majukumu mengi muhimu. Makala hii inadhamiria kuzichunguza riwaya tatu teule za mwandishi Zainabu Burhani ambaye ni mwanamke. Tutaangazia jinsi anavyowasawiri wahusika wa kike na kama kuna athari za itikadi za kitamaduni, kisiasa na kiuchumi kwa

mwandishi huyu. Hii ni kwa sababu fasihi kama zao la jamii huchota malighafi yake kutoka katika mazingira halisi ya kiutamaduni yaliyomzunguka mwandishi. Zainabu Burhani ni mwandishi wa kike ambaye alizaliwa mwaka 1937 visiwani Zanzibar ingawa ana uraia wa nchi ya Kenya. Familia yake ilihamia Mombasa baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Kwa mujibu Mazrui (2007) Zainabu ni mmojawapo wa waandishi mashuhuri wa kike. Miongoni mwa riwaya alizoziandika ni *Ulimbo* (1976), *Mali ya Maskini* (1981), *Kikulacho* (1985), *Mwisho wa Kosa* (1987) na *Kipimo cha Mizani (*2004). Katika kazi hizi ametusawiria uhalisi wa mambo ya kijamii kupitia wahusika wake na maudhui anayorejelea. Anauthamini utamaduni wa Mwafrika pamoja na elimu ya kigeni. Burhani anasisitiza maadili na kukashifu uozo wa kijamii kama vile ufisadi, wivu na chuki. Anaangazia vilevile nafasi ya mwanamke katika jamii. Makala hii inaangazia taswira ya mwanamke katika jamii kwa misingi ya itikadi, kiuchumi, kitamaduni, kidini na ndoa. Sehemu inayofuata inafafanua kuhusu nadharia ambayo imetumika katika uchambuzi wa data za makala hii.

## 2.0 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika

Nadharia inayoongoza makala hii ni Unisai au Ufeministi wa Kiafrika. Mkabala huu hujaribu kuelezea matatizo yanayowakabili wanawake wa Kiafrika, kinachoyasababisha na jinsi ya kujiepusha nayo. Mwasisi wa nadharia hii ya Ufeministi wa Kiafrika ni Steady (1981), ametambua kuwa dhuluma ambazo zimekuwa zikimkandamiza mwanamke wa Kiafrika ni kama vile kutokuwa na uwezo wa kuchagua kuwa mzazi au mke wa mtu, ukeketaji wa wanawake, unyamavu wa kulazimishwa, unyanyasaji kutoka nje, urithi wa mila na desturi, rangi yake mwenyewe na vilevile kuonewa kwa wanawake tasa. Steady (1981) anaeleza kuwa Ufeministi unapohusishwa na fasihi ya Kiafrika unafaa kuchunguza hali za kijamii na kiutamaduni zinazochangia katika unyanyasaji wa wanawake wa Kiafrika. Makala hii imetumia mihimili ifuatayo ya nadharia hii kwa mujibu wa Steady (1981):

a) Mwanamke wa Kiafrika ana uwezo wa kujitegemea na kuishi bila ya kudhulumiwa;
b) Mwanamke wa Kiafrika ana nafasi kubwa katika ujenzi wa jamii ambayo yeye ni mshiriki;
c) Mwanamke wa Kiafrika anaweza kuwa shujaa na hata mtawala;
d) Uhalisia wa wanawake wa Kiafrika unadhihirika katika fasihi ya Kiswahili.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa Ufeministi kwa jumla ni nadharia ambayo imewekewa misingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na

kiuchumi. Wamitila anaeleza kuwa hii ni nadharia ambayo inasaili na kudadisi misimamo na itikadi ya kiume ambayo imekuwako katika jamii kwa kipindi kirefu.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999) wakirejelea mawazo ya Cheri Register, mmoja wa waasisi wa nadharia hii katika kitabu cha Ruthven (1990), wanasema kuwa nadharia hii:

a) Hutumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali inayomkumba mwanamke ili iweze kueleweka na watu wengi;
b) Hunuia kuwasawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na jinsia. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu bila kujali maumbile;
c) Huhamasisha wasanii wa kazi za sanaa ili wawe na wahusika wa kike ambao ni vielelezo wenye uwezo wa kuigwa na wasiotegemea waume kujitambulisha;
d) Huona kuwa jinsia ni mojawapo ya mambo muhimu ambapo mahusiano ya kijamii yanajengeka. Maisha yetu ya baadaye yanategemea kama tunazaliwa wanaume au wanawake;
e) Hufufua fasihi ya kike katika fasihi ya Kiswahili kwa kuweka wazi kazi za sanaa zilizotungwa na wanawake na ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume.

Naye Ogundipe-Leslie (1984) anaeleza kuwa matatizo yanapomkumba mwanamke wa Kiafrika huonyesha uoga, mielekeo ya kutaka kuwafurahisha wengine na kubembeleza badala ya kutenda vitendo vya kutetea haki. Aidha, Kohrs-Amissah (2003) katika tahakiki ya riwaya tatu zilizoandikwa na waandishi wa kike (Aidoo, 2004; Emecheta, 1994; Darko, 1998), anasema kuwa Ufeministi wa Kiafrika haujihusishi tu na kusuluhisha matatizo kati ya wanawake na wanaume; kwani kuliondoa tatizo moja hakutasuluhisha matatizo yanayowakumba wanawake wa Kiafrika. Hata usawa ukiwapo kati ya wanaume na wanawake, matatizo kama vile athari za kikoloni na ubaguzi bado yatakuwapo. Ufeministi huu wa Kiafrika vilevile huchunguza asasi zilizo katika jamii za Kiafrika ambazo zinamthamini mwanamke na kupuuza zile zinazowaletea madhara. Kwa kuwa, utunzi wa kazi ya sanaa huweza kuongozwa na itikadi iliyopo katika jamii, sehemu inayofuata inafafanua dhana hii.

## 3.0 Itikadi

Itikadi humwongoza mwandishi katika uelezaji wa matukio ya jamii anayoishughulikia na itikadi hiyo hujibainisha kwa namna anavyotoa maelezo yake au namna wahusika wanavyoingiliana kupitia kwa maudhui na dhamira yake. Mwandishi ni mja wa wakati wake, jamii yake, utamaduni wake na tabaka maalum. Itikadi kwa ujumla humwathiri mwandishi yeyote yule katika kuwasilisha maudhui yake na pia usawiri wa wahusika wake. Kimani (2003) akiwanukuu

Wellek na Warren (1949: 75) anafafanua madai haya kuwa maisha ya mwanafasihi na mazingira yake ya kihistoria, kisiasa, kijamii, pamoja na hali za kiuchumi zina uhusiano mkubwa na uandishi wa kazi zake.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), itikadi ni mfumo wa mawazo fulani ambayo ni msingi wa mwelekeo fulani wa kiuchumi au kisiasa. Anaendelea kufafanua kuwa itikadi ni mawazo ambayo yanachukuliwa au yanawahusu watu kadhaa. Itikadi katika jamii huweza kulisaidia kundi linalotawala kuudhibiti uchumi na hata njia za uzalishaji mali. Wao ndio hata huendeleza zile imani kupitia dini, elimu na utamaduni. Kwa mfano, ikiwa asasi katika jamii inawataka wanawake kuwatii waume zao basi viongozi watahakikisha kuwa itikadi hii imempa mwanamke nafasi ya pili baada ya mwanamume (Abercrombie na wenzake, 1990).

Mwandishi yeyote yule hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake kwa sababu ana masilahi katika jamii hiyo. Yeye ni mmoja katika jamii ya binadamu. Huzaliwa na binadamu, akalelewa nao, akaishi nao katika maisha yake ya kila siku na akapewa na jamii chombo cha fasihi, yaani lugha. Katika kutangamana na binadamu, mwandishi hukumbana na tajiriba zinazomsaidia katika masimulizi yake. Huona watu wakicheka, wakilia, wakiuana, wakipendana, na hata wakidanganyana. Haya yote humwathiri kwa namna moja au nyingine. Kazi yake ya fasihi ni kiungo chake na jamii anayoilenga. Mwandishi hutarajia kwamba atajumuika pamoja na hadhira yake kihisia na kisaikolojia. Kwa hivyo, hutumia umbuji kama chombo cha kutekea hisia na saikolojia ya hadhira yake. Isitoshe, kazi ya sanaa ina taathira kwa wanajamii – hutilia nguvu na kudhoofisha imani zao, mawazo yao, matarajio yao na hofu zao. Itikadi ya jamii yoyote ile hujikita katika misingi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Matukio katika jamii yoyote ile hayana utaratibu wowote bali yanaingiliana. Kwa hivyo, uchaguzi ufanywao na mwandishi utaelekezwa na falsafa yake ya maisha ambayo ndiyo msingi wa itikadi yake. Kama anavyodai Ngugi wa Thiong'o (1986: 78) kuwa:

> Jinsi mwandishi anavyouchora uhalisi wa maisha huathiriwa na falsafa yake ya kimsingi kuhusu maumbile na jamii na mbinu yake ya kupeleleza maumbile ya jamii hiyo. Jambo hili ndilo litakalomwelekeza msanii katika ubainishaji wa matukio kiuhusisho au kiutengano; katika utuvu au yakibadilika na kadhalika (tafsiri ya mtafiti).

Itikadi humwongoza mwandishi katika uelezaji wa matukio ya jamii anayoishughulikia na itikadi hiyo hujibainisha kwa namna anavyotoa maelezo yake au namna wahusika wake wanavyoingiliana kupitia maudhui yake. Mwandishi ni mja wa wakati, jamii, utamaduni na tabaka maalum. Mwandishi anaweza kufungwa na itikadi ya jamii yake anapoandika kazi yake. Ikiwa ile jamii

ni ya kuumeni bila shaka wahusika wake wa kiume watajitokeza kuwa na mamlaka katika jamii zao ilhali wale wa kike huchukua nafasi ya pili. Hata hivyo, mwandishi anaweza kuwa huru katika uandishi wake na kutowekewa mipaka ya itikadi aliyokulia ndani. Akiandika kwa kuzingatia maoni ya wafeministi, atajaribu kumnasua mwanamke kutokana na mizigo aliyobebeshwa kwa miaka mingi.

Wamitila (2002: 157) anashambulia na kukosoa asasi kama vile ndoa, dini na hata utamaduni ambazo zinachangia katika kumdhalilisha mwanamke. Mawazo kama haya yanasisitizwa pia na Millet (1977) anaposema kuwa miundo ya jamii nyingi pamoja na asasi zake vinashirikiana kumkandamiza mwanamke.

Lugha hasa ndiyo njia muhimu zaidi inayotumika katika malezi na elimu na pia katika nyanja zinazochangia utu na mielekeo ya kijamii kuhusu jinsia kwa ujumla. Kwa mujibu wa Escholz (1982) matumizi ya lugha ndiyo yanayokuza na kupalilia mawazo yenye taasubi za kiume. Ubaguzi wa kiuana hujitokeza kupitia ishara za lugha ya kitamathali katika asasi kama vile ukoo, ndoa, dini au maelezo kuhusu maumbile na matumizi mengineyo ya lugha.

Mtazamo wa kijinsia katika fasihi ya Kiafrika huhimiza kuzitafiti jamii za Kiafrika na hasa kufufua asasi, amali, mitazamo, itikadi na mila ambazo zinadhibiti usawa huu. Mtazamo huu hauigi maoni, hisia, hoja wala nadharia za kigeni bali unaheshimu na kutambua haki ya kimaumbile ya kila mwanamke kujiamulia na kujichagulia hali ya maisha yake ya kibinafsi, bila kulazimishwa. Ufemenisti wa Kiafrika unapendekeza ushirikiano kati ya wanawake na wanaume ili kuweza kuondolea mbali dhuluma dhidi ya mwanamke. Hata hivyo, itambidi mwanamke mwenyewe kuwa katika mstari wa mbele kutetea haki zake. Kabla ya kuanza uchambuzi wa data sehemu inayofuata inaangalia vitengo mbalimbali vya itikadi ambavyo vinaweza kumuathiri mwandishi katika utunzi wa kazi yake.

## 3.1 Asasi ya Kiuchumi

Wanawake hawapatikani wala kuishi nje ya jamii; wana nafasi waliyotengewa na jamii kama ‘wanawake’. Wanawake hunyanyaswa kwa msingi ya jinsia yao hasa kutokana na itikadi zinazoendelezwa na jamii husika. Hata kazi wanazotengewa huchukuliwa kuwa duni na jamii. Engels (1975) adai kuwa chanzo cha historia ya kunyonywa na kukandamizwa kwa wanawake ilianza wakati binadamu walipogawanyika katika matabaka mbalimbali. Jamii asilia ilikuwa na uthamani sawa wa kazi za wanaume na wanawake. Jamii ilipobadilika na kuwa ya kitabaka, ilianzisha urithi upande wa baba. Kutokana na ugawaji wa majukumu kazi za upande wa wanaume zilileta faida zaidi kushinda zile za wanawake.

Kutokana na haya, umilikaji wa mali ulimwendea mwanamume ukiwamo pia uzalishaji mali. Naye mwanamke alijitambulisha kwa majukumu ya uzazi na malezi. Hapa mwanamke alifaidika ingawa hangeweza kutoa uamuzi wowote kuhusu mali isiyo yake. Nafasi ya mwanamke iliendelea kuwa nyuma kutokana na

tofauti za kikazi. Tangu jadi jamii ikafunzwa kuamini kuwa mahala panapomfaa mwanamke ni nyumbani na ulezi wa watoto (Figes, 1978). Mawazo haya yanatiliwa nguvu na Tong (1989:87) anapoeleza:

> Hadi hivi majuzi mfumo wa kuumeni umemfanya mwanamke kuamini kuwa kuzaa ndiyo kazi yake ya pekee (tafsiri ya mtafiti).

Mfumo dume ulirutubishwa na umwinyi katika jamii nyingi. Haja ilikuwa ni kuhimili nguvu za mwanamume. Tong (1989: 181) akimnukuu Heidi (1989) anasema kuwa Umwinyi na mfumo dume ni mahayawani hatari ambao wanahitaji kushambuliwa kwa silaha tofauti. Anaendelea kusema kuwa kupitia kwa majukumu kugawanywa kiuana, mfumo dume ungali umempa mwanamke nafasi ya pili kazini na hata nyumbani. Kitengo hiki cha itikadi kinaweza kumuathiri mwandishi yeyote awe wa kiume au wa kike.

### 3.2 Asasi ya Utamaduni

Ndungo (1998) asema kuwa utamaduni na malezi huchukua nafasi muhimu katika kuunda na kuimarisha itikadi na mielekeo ya jamii kuhusu wanawake. Tamaduni nyingi humtaka mwanamke awe mnyenyekevu, mnyamavu, mpole na mtiifu wala asiwe na hiari katika maisha yake yote ya kujichagulia au kujiamulia lolote lile.

Jamii hukuza msingi wa tabia na mtazamo wa watu wake. Hivyo basi, mwanamke huzingatia mielekeo na itikadi za jamii anamoishi hata kama ina mfumo dume. Wamitila (2002: 157) akimnukuu de Beauvoir (1963) anatoa kauli kuwa utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Inamchukulia mwanamke kama kitu hasi naye mwanamume kama binadamu kielelezo. Mwishowe mwanamke anaishia kuwa kama chombo cha mfumo wa jamii cha kuendeleza utamaduni huo hasi.

Lugano (1989) anasema kuwa jamii nyingi za Kiafrika hupendelea zaidi wanawake wanaozaa watoto wa kiume. Anaendelea kudai kuwa unyonge wa mwanamke umemfanya kuwa kisingizio cha kila jambo bovu linalotokea katika ndoa. Ikiwa mwanamke amezaa wasichana pekee, kosa linakuwa lake, ikiwa hakuzaa kabisa pia ni kosa lake. Hata wanaume walioelimika na kufahamu elimu ya uzazi wanaendeleza hii itikadi.

Ndoa katika jamii nyingi za Kiafrika huchukuliwa kuwa imekamilika iwapo mwanamke amezaa mtoto hasa wa kiume, ambaye huchukuliwa kama nguzo ya jamii (Kimani, 2003: 19). Tatizo hili linazorotesha maendeleo ya jamii katika nchi nyingi zinazoendelea. Watu wanalazimika kupata watoto wengi wasioweza kuwalea hasa wanapojitahidi kupata wa kiume. Umuhimu wa kuwa na mtoto wa kiume unathaminiwa na jamii kiasi cha kutoyajali maisha ya mama mzazi. Wanawake wenyewe wameikubali hali hii jinsi ilivyo. Kwa mujibu wa Wamitila (2002: 160):

> Utamaduni umeundwa au kujengwa kwa namna inayomkandamiza mwanamke katika nyanja zote za maisha. Wanawake wanapokulia katika jamii zao wanayachukua mawazo yanayoendeleza itikadi hii hasi na kwa njia hii kuidharau jinsia yao wenyewe.

Katika jamii nyingi za Kiafrika wanawake walihitajika kujiremba ili kuwafurahisha waume zao. Momanyi (1998) akimnukuu Knappert (1979: 84) asema kuwa jukumu la mwanamke lilikuwa kujiremba na kujinadhifisha mbali na kuitunza jamii yake, mume na watoto. Mke alipaswa kujipamba kwa kila hali ili aweze kuajabiwa na mumewe. Haya ni mafunzo yaliyojikita katika mfumo dume. Wanawake walichukuliwa kama mali ya waume wao.

### 3.3 Asasi ya Dini

Dini ni mojawapo ya asasi ambazo zinamtukuza mwanamume na kumdunisha mwanamke. Msimamo wa dini nyingi kuhusu nafasi ya mwanamke umesaidia sana kuwachochea wanaume kuwa wazembe zaidi. Dini inawathibitishia kwamba Mungu alimuumba mwanamke kwa minajili ya kumsaidia mwanamume katika harakati zake za kupambana na matatizo ya kidunia. Dini za Kikristo na Kiislamu zina mizizi yake Mashariki ya Kati na Uarabuni ambako mila na desturi zao zinaendeleza mfumo dume (Masinjila, 1997: 1).

Kwa kutumia misingi ya dini ya Kikristo mwanamke yuko chini ya mwanamume. Anahitaji kumtii na kumnyenyekea mumewe kama asemavyo Mtakatifu Paulo anapoandika Waraka wa Waefeso (5: 22-25) katika Biblia Takatifu:

> Enyi wake watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wanawatii waume zao katika kila jambo.

Dini imempa mwanamke nafasi ya pili baada ya mwanamume. Momanyi (1998: 90) akimnukuu Alamin bin Ali Mazrui katika Strobel (1979: 55) anabainisha haya:

> Mungu alituumba wanaume kwa wanawake na kwa sababu ya uovu wa mwanamke, alimjaza mwanamke unyonge wa mwili na akili. Alimpa mwanamume uzuri wa nguvu, akili na mawazo mema, na kutokana na hili ndipo akataka wanaume wawasimamie wanawake na kuwalinda…wanawake pia hawana makosa kwa yale wayafanyayo kwani hawajui lolote. Lakini makosa yote ni juu ya wanaume wanaojua uzuri na ubaya…

### 3.4 Asasi ya Ndoa

Wamitila (2002: 157) anasema kuwa ndoa ni asasi mojawapo ya kitamaduni inayoendeleza ukandamizwaji wa wanawake. Asasi yenyewe imejengwa kwenye

imani ya uwezo mkubwa alionao mwanamume na kuishia kumwangalia mwanamke kama chombo tu.

Kiburi cha mwanamume hujitokeza hapa. Jamii inaamini kuwa mwanamke anapoolewa anakuwa mojawapo ya mali zinazomilikiwa na mwanamume. Mahari inapotolewa inamfunga mwanamke kwa mumewe. Hata akiteswa anavumilia kwa sababu akitoroka wazazi watahitaji kurudisha mahari. Mahari inatumiwa kama mnyororo unaomfunga mwanamke hasa wa Kiafrika. Kama asemavyo Matteru (1982: 16):

> Mahari yanayolipwa kwa wazazi wa msichana yanatilia nguvu utumwa wa msichana, ambaye sasa hawezi kamwe kumtoroka mumewe na jamii yake hata wawe watesi namna gani, hasa ikiwa hawezi kurudisha mahari ambayo tayari imekwishaliwa na wazazi wake (tafsiri ya mtafiti).

Katika jamii nyingi za Kiafrika mwanamke anahitaji kumnyenyekea, kumtii na kumpendeza mumewe. Mawazo haya yanahimizwa na Mwana Kupona akimshauri bintiye katika *Utenzi wa Mwana Kupona* (1858) akinukuliwa na Mulokozi (1999). Anamwambia bintiye jinsi ya kumhudumia mume wake katika maisha ya ndoa. Anamshauri bintiye amfanyie mumewe kila limpendezalo hata kama yeye mwenyewe linamchukiza. Katika utenzi aliomwandikia anamwambia:

> Na ukitaka kutoka
> Sharuti rukhusa taka
> Uonapo meudhika
> Rudi na kuikalia (ubeti 44)

Mwana Kupona anamtarajia bintiye anapotaka kuondoka pale nyumbani apate ruhusa kutoka kwa mumewe. Ikiwa mumewe atakataa basi asiondoke. Taswira ya mwanamke inaonyesha mfungwa asiye na uhuru wowote. Asasi ya ndoa katika jamii nyingi za Kiafrika huendeleza dhuluma dhidi ya mwanamke. Humpa nafasi ya pili baada ya mwanamume. Kwa sababu ya wingi wa itikadi zinazotetea mfumo dume, mwandishi wa kike anaweza kujikuta ameathiriwa na itikadi hizi.

## 4.0 Usawiri wa Mwanamke wa Kiafrika katika Riwaya Teule

Jamii nyingi za Kiafrika zilifuata mfumo dume. Mpangilio katika jamii za mfumo huu hudhihirisha muundo thabiti wa kuwezesha mamlaka ya kiume. Itikadi hii inamfanya na kumlazimisha mwanamke kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni. Katika mfumo huu majukumu huwa tayari yamegawanywa. Ufemenisti wa Kiafrika unatambua uhusiano wake na unisai wa kimataifa lakini unafafanua unisai ambao una mahitaji na malengo maalumu yanayotokana na uhalisi wa maisha ya wanawake katika jamii za Kiafrika. Mwanamke katika riwaya teule za Burhani amesawiriwa kama mzazi na mlezi, mnyenyekevu na asiye na uwezo wa kujiamulia.

## 4.1 Mwanamke kama Mzazi na Mlezi

Katika jamii nyingi za Kiafrika wajibu wa mwanamke ulikuwa ni kuwalea watoto kwa kuwapikia, kuwatunza na kuwafunza tabia nzuri. Jukumu lake kama mzazi ni jambo linalokubalika katika jamii za ulimwengu. Mwanamke hulelewa, kuelimishwa na kutayarishwa kwa jukumu hili muhimu. Mfano mzuri ni malezi ya mtoto wa kike katika jamii ya Waswahili ambayo yanashikilia kwamba mtoto huyu hana budi kuwa mke na mama bora wa siku za usoni (Inyani, 1994: 26). Mwanamke kama mzazi na mlezi anabebeshwa mizigo mingi. Katika riwaya ya *Mali ya Maskini* (1981) tunaona kwamba Zahara na wadogo zake hawapendi kuzifanya kazi za nyumbani. Kila mara kuna ushindani kati yao. Kwa hivyo mama yao ambaye ni Siti huamua kuzifanya kazi hizo:

> Kwa hivyo mama yao alivyokuwa amechoshwa na ugomvi na ushindani wa kila siku, alihiari kuzitekeleza mwenyewe kazi hizo na ndiyo maana hakuwa hata na wakati mapumziko (uk. 5).

Katika jamii hii majukumu yanagawanywa kwa msingi wa kijinsia. Hii ndiyo sababu Kadiri yuko katika duka lake akiuza, wakati Siti anafanya kazi za nyumbani. Matarajio yetu ni kuwa watoto watamsaidia mama yao kazi pale nyumbani. Zahara haelewi wajibu wao katika jamii.

Nadharia ya Unisai inatambua kuwa utamaduni unachangia sana katika kunyanyaswa kwa mwanamke wa Kiafrika. Utamaduni huu umemfanya mwanamke kama kiumbe cha kutoa huduma kwa wengine na zaidi watoto na mumewe. Hakuna wakati yeye anafurahia huduma kutoka kwa mwanamume. Mwanamke katika jamii ya Kiafrika anahitajika kuijali familia yake kuhakikisha kuwa wamepata lishe. Katika *Mwisho wa Kosa* (1987) tunamwona Keti akishughulikia familia yake:

> Keti alirejea kwake ili akayatayarishe chakula cha usiku kwa sababu ya mumewe na mtoto wake mmoja wa kike (uk. 18).

Taswira inayojitokeza hapa ni ugawaji wa kazi kiuana katika jamii nyingi za Kiafrika. Jamii huwa na matarajio maalum kwa mwanamke yeyote anayeolewa. Kwa mujibu wa malezi ya aina hii wanawake wanalazimika kuuficha utu wao halisi. Nafasi wanayopewa ni ya pili. Wanawake lazima waungane na kupambana ili kubadilisha hali ilivyo. Katika *Mwisho wa Kosa* (1987) Muna anasema kwa maoni ya waume:

> Mwanamke kazi yake kukaa nyumbani, kupika, kufua, kuzaa na kulea. Ana haja gani tena ya masomo? (uk. 127).

Haya ni mawazo yaliyokita mizizi katika itikadi nyingi za Kiafrika. Wanawake wengi wameikubali hali hii. Baba anamtahadharisha Muna:

> Usifikirie kuwa wanawake wote watakuwa upande wenu. La wengi watakupingeni! Kwa sababu hayo ndiyo mazoea yao na malezi (uk. 128).

Tatizo kubwa zaidi ni wanawake wenyewe. Wanawake wanakosa kuzungumza kwa sauti moja. Hawana umoja na ushirikiano. Steady (1981) ana maoni kuwa wanawake wa Kiafrika wanakubali matatizo yanayowakabili na mambo wanayotendewa na kuona kuwa ni majaaliwa ya Mungu hivyo hakuna lolote la kufanya. Mwandishi Burhani amejikuta katika itikadi ya mfumo wa kuumeni. Hatuoni akiwapa wanawake nafasi ya kuweza kushirikiana ili wajikomboe. Vita vinavyojitokeza ni vya mhusika binafsi kama vile Muna kujaribu kujikomboa.

Uzazi ulidhihirisha baraka katika jamii. Mwanamke tasa huzomewa ilhali yule anayezaa watoto wa kike kosa linakuwa lake. Hii ni dhuluma kubwa ambayo imekuwa ikitendewa wanawake. Hata wanaume ambao wameelimika na kufahamu elimu ya uzazi huchangia katika lawama hiyo. Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* (2004), Amini alifurahi sana mkewe Halima alipojifungua mtoto wa kiume. Mwandishi anaeleza:

> Wakati huu Halima alizaa mtoto wa pili wa kiume. Amini alifurahi sana, akampa mtoto huyu jina la Uledi (uk. 33).

Mwandishi Burhani anaonyesha kuwa hakuna usawa kati ya watoto wanaozaliwa. Anawatukuza wa kiume kuliko wa kike. Utamaduni mkongwe hautambui thamani ya mtoto wa kike.

Mariyamu katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* (2004) alijitokeza kuwa mlezi mzuri kwa wanawe. Tunaambiwa:

> Asubuhi aliwaamsha wale watoto wake wawili, akawakogesha, akawavalisha nguo, wakati mtumishi akiwatayarishia chakula cha asubuhi na mikoba yao ya shule (uk. 104).

Rehema vilevile katika riwaya hii anajitolea kuwalea watoto watatu wa Halima ambao walitoroka kutoka kwa baba yao mdogo Umari ambapo waliyapata mateso mengi na hata kunyimwa haki ya kusoma. Tunaelezwa:

> Rehema aliwaangalia vizuri, na kusema nao kwa upole na walimsikiliza na kumtii. Walikubali kwenda shule kuendelea na masomo yao (uk. 191-192).

Mwandishi Burhani anamsawiri mwanamke wa Kiafrika kama mzazi na mlezi katika familia yake.

## 4.2 Mwanamke ni Mnyenyekevu

Taswira hii ya unyenyekevu imechorwa na mwandishi Burhani kupitia wahusika wake. Katika *Mwisho wa Kosa* (1987) Muna anapoolewa na Hassan ananyimwa uhuru wa hata kuwatembelea wazazi wake. Anapomwambia mama yake anamjibu:

> Mwanangu, najua kuwa hayo yanakukera, wala sisi hatufurahi nayo lakini umtii mumeo, usimvunje mkakosana bure (uk. 224).

Hapa Muna anatakiwa kumtii na kumnyenyekea mumewe ingawa hayapendi mambo anayotendewa. Burhani hakemei tabia ya Hasani. Ingawa Rashid anakosa kwa kuishi na Monika, hilo halichukuliwi kama kosa. Mama yake Salama anamwambia kuwa Rashid ni mwanamume kwa hivyo anakubalika kukosa. Mama anamshauri Salama kuwa:

> Lazima ujue kuwa katika maisha mwanamke ndiye mwenye mzigo mkubwa na mzito wa kusubiri na kustahimili na kusamehe siku zote na **kunyenyekea** (msisitizo wetu) (uk. 234).

Monika mwanzoni anapotoka Ulaya amejawa na kiburi. Anapuuza ushauri wa wazee wake na hata kutoroka nyumbani kwenda kuishi mjini. Huko mjini mambo yanapomwendea kombo anarudi nyumbani. Anakuwa kama ng'ombe anayevunjika mguu malishoni ambaye hurejea zizini kusaidiwa. Monika mwishowe anarejea nyumbani na kunyenyekea mbele ya wazazi wake na hata kukubali kuozwa mume:

> Hakuona fahari kwa yale aliyoyafanya. Alijua huzuni aliyowasababishia wazee wake. Alimgeukia baba yake na kusema, 'Nimekubali' (uk. 26).

Katika riwaya ya *Mali ya Maskini* (1981) Kadiri alimtuma mwanawe Ali akachukue kikapu kimoja na sanduku. Lakini akasahau kwenda. Lawama yote ikamwangukia Siti ambaye aliamua kunyamaza na kutojibu lolote. Kadiri anamwambia:

> Yote ni wewe. Unawaharibu hawa kwa kuwadekeza kwako, na kila nikikwambia hunisikilizi. Siti aliguna tu bila ya kujibu lolote maana maarifa yake yalimwambia afadhali amalize joto lake (uk. 3).

Unyamavu wa kulazimishwa ni baadhi ya dhuluma anazotendewa mwanamke wa Kiafrika (Steady, 1981). Siti ana hiari kutomjibu mumewe hata kama anajua ukweli upo wapi. Utamaduni haumruhusu kufanya hivyo. Kulingana na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika anafaa atambue kuwa yeye tu ndiye anayeweza kuufasili uhuru wake wa kujua kile hasa anachohitaji. Zahara ana hamu ya kwenda kuangalia mashindano ya mpira na wenzake shuleni. Babake anapomnyima ruhusa ya kwenda huko anamtaka akae pale amsaidie mamake. Anayatii haya na kubaki pale nyumbani kutayarisha chakula.

Bakari anapoamua kumchukua Zahara, binti wa nduguye Kadiri, ili aishi kwake na amsaidie kulipa karo, mkewe halipendelei jambo hilo. Bakari anasisitiza Kadiri ndiye aliyemlea, akamsomesha na kumpa kazi na pia kumuoza mke. Kwa hivyo ni sharti amsaidie. Anamwambia Imani:

> Juu ya hayo nilikushauri kutaka kujua fikra zako na nimekwishaamua kuwa atakuja kukaa hapa, ukitaka usitake (uk. 32).

Hapa Imani analazimika kumtii na kumnyenyekea mumewe Bakari.

Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* (2004), Burhani anatuonyesha jinsi unyenyekevu wa Halima ulivyoepusha ugomvi kati ya ndugu wawili - Amini na Umari. Halima alijua kuwa Umari hampendi na hata wakati mwingine ile heshima ya kishemeji hawezi kumpa. Mwandishi anaeleza:

> Halima alistahamili hayo kwani hakupenda kugongana naye wala hakupenda kuleta ugomvi baina ya Amini na ndugu yake (uk. 42).

Unyenyekevu wa Halima unaonyesha udhaifu kwa upande wa mwanamke. Badala ya kutatua tatizo ananyamaza hata kama angelikuwa na suluhisho. Burhani anamsawiri mwanamke kwa mtazamo hasi kama kiumbe asiyeweza kutoa maoni yake. Anajitokeza kama mtegemezi. Jambo hili linapingwa na Nadharia ya Ufeministi ambapo mwanamke anafaa kujitegemea ili kuiondoa minyororo iliyomfunga. Jamii nyingi za Kiafrika hazimpi mwanamke nafasi katika baadhi ya shughuli za kijamii. Utamaduni na dini, zikiwamo za Kikristo na hata Kiislamu, zinamhitaji mwanamke awe mnyenyekevu mbele ya mumewe. Gitau (2005) akimnukuu Uchendu (1993: 53) anasema kuwa katika jamii nyingi za Kiafrika wanawake hawakupewa sauti ya kusema lolote. Walihitajika kukaa nyumbani ilhali wanaume walielimishwa na baadaye wakashika vyeo mbalimbali serikalini.

### 4.3 Mwanamke ni Kiumbe Asiye na Uwezo wa Kujiamulia

Katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* (1987), Keti anakumbuka jinsi umaskini ulivyomsukuma mumewe, ambaye ni marehemu, kumuoza binti yao wa pekee. Anafanya hivi bila hiari ya binti wala Keti mwenyewe. Anaozwa akiwa na umri mdogo sana. Keti anakumbuka:

> Baba yake alimwoza mume alipokuwa na umri wa miaka kumi na minne na kumpeleka kwa mumewe (uk. 31).

Ufemenisti wa Kiafrika unapinga mwanamke kutokuwa na uwezo wa kuchagua kuwa mke wa mtu. Bi Keti anahuzunishwa na suala hili la mumewe kumuoza binti yao mdogo. Katika jamii za Kiafrika mwanamke hana kauli katika ndoa. Burhani alipaswa kulipinga wazo hili la kuozwa mapema na kwa lazima kwa binti huyu lakini hatumuoni akifanya hivyo.

Mamake Ali siku moja ghafla anatulia na kumwangalia Zahara. Haja yake ikiwa ni ampose kwa ajili ya mwanawe Ali, anamwambia;

> Mashallah! Zahara mwanangu umekuwa mkubwa sasa. Umekuwa wa kuolewa tena. Ama miaka inakwenda! (uk. 53).

Uchumba kati ya Rashid na Salama unapangwa na wazazi wao walipokuwa wachanga. Monika anapoanza uhusiano kati yake na Rashid anajaribu kumshawishi aachane na huo uchumba. Monika anamwambia Rashid;

> Madhali uchumba huo ulipangwa na wazee tu - hapakuwa na mapenzi baina yake na Salama, hakuona kuwa Rashid amelazimika kuyakubali hayo au kufungika na uchumba asioutafuta (uk. 57).

Ingawa Muna anaposwa na wazee wa Hasani, tunamwona babake akimpa nafasi ya kuyafikiria mambo hayo kabla ya kuamua kuolewa na Hasani. Anaamua kuyafuata ya wazee wake. Mwandishi anasema:

> Yeye aliona kuwa jambo hili lilimbidi na baada ya kuona kuwa wazee wameyakubali na kuwa Hasani hakuwa na hila yoyote kubwa au ya kuchukiza hakujitaabisha tena kuyafikiri (uk. 63).

Monika alishangaa kwa nini Muna anakubali kuolewa na mtu aliyechaguliwa na wazee wake. Anamwambia Muna:

> Mambo ya kizamani. Wazee wetu waliona hivyo ndivyo lakini sasa dunia imeendelea na watu wanabadilika. Lazima watu wajuane, wapendane, kwanza ikiwa wanataka kuishi pamoja (uk. 55).

Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* (2004) Halima anapokea posa kutoka kwa Amini na kukubali kuolewa naye. Bibi yake Halima aliyekuwa hai wakati huo alifurahi kupokea posa za Amini. Anamwambia Halima:

> Mjukuu wangu, umebahatika! Maana katika dunia hii ya leo ni wachache sana walio na tabia nzuri za kijana huyo. Fikiri vizuri. Mimi ningekushauri umkubali! (uk. 29).

Baada ya mumewe Amini kufariki, Halima anapokea posa kutoka kwa Selemani naye anakubali kuolewa naye. Inaelezwa na mwandishi kuwa:

> Mzee Hasani alimletea habari za furaha, kuwa Halima amekubali posa za Selemani lakini hakutaka sherehe wala ghasia zozote (uk. 231).

Salama naye kufikia mwisho wa riwaya anapokea posa kutoka kwa Daktari Isa. Naye anakubali kuolewa naye. Anamwambia Halima:

> Kweli, basi ameniposa, na harusi itakuwa karibu. Baada ya miezi mitatu tu (uk. 232).

Katika riwaya ya *Mali ya Maskini* (1981) tunamwona Selemani, ambaye ni Waziri katika Wizara ya Mambo ya Biashara, anamposa Zahara. Ali, kakake Zahara, anaulinganisha umri wa Selemani sawa na wa babake kwa hivyo halipendelei wazo hilo. Zahara anapewa nafasi ya kujiamulia mwenyewe. Bakari babake Zahara anasema:

> Kama atakavyoamua ni mtoto wetu. Itatubidi tumwangalie kwa kila litakalotokea (uk. 93).

Mwandishi Burhani anaonyesha kuwa mwanamke anaweza kupewa uhuru wa kujichagulia mume kama afanyavyo Zahara. Badala ya kuolewa na mzee Selemani anaamua kuolewa na Yusuf. Burhani hapa anaonyesha kuwa mwanamke anaweza kujikomboa na kuwa huru.

## 5.0 Hitimisho

Usawiri wa mwanamke katika riwaya hizi tatu za Burhani umegubikwa na mfumo dume. Hali hii inatokana na malezi ya mwandishi katika jamii yake. Katika kazi hizi kuna wanawake ambao wanaonyesha uhalisi wa mwanamke wa Kiafrika. Mwandishi amemsawiri mwanamke kama mzazi na mlezi. Katika jamii nyingi za Kiafrika jukumu la mwanamke ni kuozwa, kuingia katika maisha ya unyumba na kuendeleza kizazi. Kuozwa ilikuwa hatima ya mtoto wa kike. Alihitaji kuvumilia dhiki katika ndoa hiyo hata kama anadhulumiwa na mumewe. Burhani anatoa kauli kwamba wazazi wahusishwe katika mipango ya ndoa ingawa uamuzi wa mwisho uachiwe watoto wenyewe. Nadharia iliyoongoza utafiti huu imelenga kuondoa ubaguzi uliojengwa katika misingi ya uana, kutupilia mbali utawala wa mwanamume asiyethamini usawa wa kijinsia. Ufeministi hujaribu kutupilia mbali mambo yote yanayomweka mwanamke katika hali duni kwa kupigana na pingu za kitamaduni, kidini, kisiasa, na kiuchumi, ambazo zimemfunga mwanamke asiendelee.

## Marejeleo

Abercrombie, N. et al.(1990). *Dominant Ideologies*. Cambridge: Unwin Hyman.
Aidoo, A. (2004). *Changes: A Love Story*. Accra: Feminist Press.
Bottomore, T. (ed). (1983). *A Dictionary of Marxist Thought*. Cambridge: Harvard University Press.
Burhani, Z. (1981). *Mali ya Maskini*. Nairobi: Longhorn.
______(1987). *Mwisho wa Kosa*. Nairobi: Longhorn.
______(2004). *Kipimo cha Mizani*. Nairobi: Longhorn.

Darko, A. (1998). *The Housemaid*. Accra: Feminist Press.
Engels, F. (1975). *The Origin of the Family Private Property and the State*. New York: Pathfinders Press Inc.
Emecheta, B. (1994). *Second Class Citizen*. Accra: Feminist Press.
Escholz, P. (1982). *Language Awareness*. New York: St. Martin's Press.
Figes, E. (1978). *Patriachal Attitudes*. London: Virago Press.
Heidi, H. (1989). *Capitalism and Women's Work in the Home*. UMI, Dissertation Information Science.
Kimani, C. (2003). Swala la Dhuluma dhidi ya wanawake katika Fasihi Andishi ya Kiswahili.Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, (Haijachapishwa).
Kohrs-Amissah. (2003). *Aspect of Feminist and Gender in the Novels of Three West African Women Writers* (Aidoo, Emecheta, Darko). Heidelberg: Books on African Studies.
Lugano, R. S. (1989). Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi, (Haijachapishwa).
Masinjila, M. (1977). *Patriarchy and women's Participation in Kenya*: Publication of Collaborative Centre for Gender and Development Responsive Politics. Nairobi: The Fredrick Ebert Foundation.
Matteru, M.L.B. (1982). The Images of Women in Tanzania Oral Literature: A Survey, *Kiswahili* Vol. 49/2.
Mazrui, A.M. (2007). *Swahili Beyond the Boundaries: Literature, Language and Identity*. Ohio: Ohio University Press
Momanyi, C. (1998). Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya PhD. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).
Mulokozi, M.M. (mh.) (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
Ndungo, C.M. (1998). Images of Women in Gikuyu Oral literature: A Case of Gikuyu and Swahili Proverbs. Unpublished PhD Thesis. Kenyatta University.
Ngugi, wa Thiong'o (1986): *Decolonising the Mind: The Politics of Language in Africa Literature*. London: James Currey Ltd.
Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
Ogundipe-Leslie, O. (1994). *African Women and Critical Transformations*. Trenton: African World Press.
Ruthven, K.K. (1990). *Feminist Literary Studies: An Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press
Steady, F.C. (1981): *Black Women Cross- Culturally*. Cambridge: Scherkman Publishing Co.

The Bible Societies. (1971). *The Holy Bible*. New York: Collins Bible.
Tong, R. (1989). *Feminist Thought*: *A Comprehensive Introduction*. Colorado: West View Press.
Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
______(2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.